

SAGCOT
SOUTHERN AGRICULTURAL GROWTH CORRIDOR OF TANZANIA

# Ubia Mkakati wa zao la Nyanya

## Muhtasari

Nyanya ni miongoni mwa zao la mbogamboga linalolimwa kwa kiasi kubwa nchini Tanzania, ambapo zinalimwa  maeneo mengi ya nchi hii kwa kiwango kikubwa na wakulima wadogo. Hata hivyo, aina ya mbegu za nyanya zinazolimwa Tanzania haziwezi kustahimili wadudu na magonjwa na hutoa mavuno kidogo. Zaidi ya hayo, nyanya ni rahisi kupasuka na hivyo basi ni rahisi kuharibika wakati wa kusafirisha. Kwa sababu hii, pia nyanya ni zao ambalo linadumu katika hali yake kwa muda mfupi sana kabla ya kuharibika. Kusaidia ukuaji wa mnyororo wa thamani wa nyanya ambao utasaidia kuondoa vikwazo katika uzalishaji nyanya na kuwapatia faida wakulima wadogo,  SAGCOT ilianzisha ubia mpya mwezi Mei 2015: Ubia wa Nyanya, unaoendeshwa katika kongani ya Ihemi ( unaojumuisha mikoa ya Iringa na Njombe).

Darsh Industries, ni msindikaji wa nyanya tangu mwaka 2015.
Kiwanda hiki kilichopo Iringa kina uwezo wa kusindika tani 200 za nyanyaghafi  kwa siku.

Kampuni ya Darsh Industries tayari inafanya kazi na wakulima wadogo na viongozi wa vijiji vinavyozunguka kongani hii kubaini wazalishaji wa nyanya na ujenzi wa vituo 8 vya kukusanya nyanya umekwisha kamilika. Vituo vya kukusanya nyanya ni nguzo muhimu sana ya ubia, vinasaidia kuongeza uwezo wa wakulima wa kupanga bei , kwa sababu hawalazimiki tena kuuza nyanya kwa bei ya chini ambayo hupangwa na wanunuzi wa kati au madalali.

Nyanya huzalishwa zaidi kwenye maeneo  oevu na kandokando ya mito, ubia wa nyanya pia umeweka kipaumbele kwenye kutumia  teknolojia endelevu za uzalishaji ili kuhakikisha ongezeko linalotarajiwa kwenye uzalishaji wa nyanya linaleta athari chanya za kimazingira. Idadi ya asasi kadhaa zinazosimamia uhifadhi wa mazingira zinashirikiana na wabia wa SAGCOT kuhakikisha kuwa kilimo cha nyanya ni rafiki kwa mazingira. Kupitia Kikundi cha Rejea Kijani (Green Reference Group) asasi wanachama, na asasi zinazoshughulika na masuala ya jamii na mazingira zinatoa mwongozo wa kiuweledi kuhakikisha kuwa kazi na shughuli zote zinazingatia kilimo endelevu cha nyanya.

Mnamo mwezi Septemba 2015, Kituo cha  SAGCOT kilitisha mkutano wa wadau mjini Iringa kuandaa mpango kazi wa kwanza wa utekelezaji wa Ubia Mkakati wa Nyanya, kuanzia wakati huo mpaka sasa mikutano ya wadau imeendelea kufanyika.

## The Southern Agricultural Growth Corridor of Tanzania (SAGCOT)

Mpango wa SAGCOT ni ubia kati ya sekta ya umma na binafsi unaolenga kuchochea Uwekezaji kwenye Kilimo biashara katika ukanda wa kusini mwa Tanzania.  Kituo cha SAGCOT kinafanya kazi kama dalali wa ubia na kitovu cha habari kwa wabia wa SAGCOT katika kuwezesha uwekezaji kwenye minyororo ya thamani inayoshirikisha  jamii na kuzingatia uhifadhi endelevu wa mazingira.Kila mwaka, aina mbali mbali za ubia mkakati zimeibuka ambazo mpango wa SAGCOT unashiriki kikamilifu kukuza na kuwezesha kutokana na matukio makuu na yanayoweza kupanua shughuli hizi.

## Nini kinasababisha Ubia wa Nyanya kuwa Ubia Mkakati?

· **Kubadilisha hali ya usalama wa chakula kwa wakulima na kuboresha hali ya maisha katika kaya.**
Ubia wa Nyanya unalengo la kuongeza tija ya uzalishaji na kisha faida kwa wakuma wa nyanya mkoani Iringa.
· Kutafuta suluhisho la kudumu katika mnyororo wa thamani
Ubia wa nyanya ulianzishwa kimkakati ili kujumuisha wadau kutoka kila eneo linalohusisha  na mnyororo huu
· **Kuwakutanisha wabia**
Wadau 14 wamekuwa wakishughulika na kuanzisha ubia, na wengi zaidi wanahimizwa kujiunga, hususan wazalishaji wa kati, wasindikaji, wafanyabiashara wa rejareja, watoa huduma yenye teknolojia bobezi na wote walio tayari kuwasaidia wakulima
· **Athari pana**
Ubia wa nyanya unatarajia kuwafikia wakulima wadogo 10,000
· **Kuonyesha athari chanya za kimazingira**
Wabia hufanya kazi na wakulima kuinua tija kwenye uzalishaji kwa namna ambayo inazingatia usimamizi wa mali asili, ikijumuisha kuyatumia tena maji yaliyokwisha tumika awali kwa kiwango cha asilimia (90%).



## Wadau muhimu kwenye Ubia wa Nyanya

- Darsh Industries
- Green Valley Agro
- TAHA
- LGAs mikoa ya Iringa na Njombe
- RAS – mikoa ya Iringa na Njombe
- WWF
- BRITEN
- INCOMET
- MUVI
- Yara
- Syngenta
- Balton
- Kisolanza
- PAWAGA Farmers Association

## Athari jumuishi na endelevu

Ubia wa nyanya umewezesha kupunguza utegemezi wa kununua toka nje ya nchi tishu laini (pulp) kama malighafi inayotumika katika usindikaji wa nyanya: Kampuni ya Darsh Industries imekuwa ikiagiza tishu laini kama malighafi kwenye usindikaji wa nyanya kwa asilimia (70%) toka nchini China kwa sababu ya kutokuwepo na wazalishaji hapa nchini. Ubia hu umeweza kuwaingiza wakulima wenyeji kwenye mnyororo wa thamani wa nyanya, kuwapatia mnunuzi wa uhakika wa kwa mazao yao ya nyanya wanayozalisha huku ukiwasaidia kuongeza tija wenye uzalishaji na kuongeza ubora kupitia mlolongo wa huduma mbalimbali za kuwasaidia. Kampuni ya Green Valley Agro inaongoza katika kuendeleza kilimo cha kiikolojia kwa wakulima wadogo wa zao la nyanya.

Ili kushughulikia changamoto zinazojitokeza kwenye maendeleo ya tasnia ya nyanya, Ubia umefanya kazi/shughuli mbalimbali kuhakikisha utekelezaji unazingatia mbinu bora za kiutendaji. Mbinu hizi zinajumuisha: kuwaunganisha wakulima na taasisi za kifedha ili kuweza kupata vifaa vya umwagiliaji, elimu kuhusu athari mbaya zitokanazo na matumizi yasiyo sahihi ya kemikali za kilimo, kujenga uwezo kwa wakulima juu ya elimu kwenye masuala ya fedha; na kujenga muunganiko wa watendaji ndani ya mnyororo wa thamani wa nyanya ili kushughulikia tatizo la ukosefu wa uratibu miongoni mwa watendaji hao uliopo kwa sasa.

## Changamoto na Hatua Zitakazochukuliwa

Uzalishaji una tija ndogo kwa sasa kuliko mahitaji ya nyanya katika ukanda. Zaidi ya hayo, mapungufu yanayoikabili miundombinu kama vile utumiaji wa miundombinu ya umwagiliaji, nishati na mtandao wa barabara vinasababisha kutokuwa na ufanisi wa hali ya juu kama inavyopaswa, pia upotevu wa mazao baada ya mavuno vinaongeza gharama ya uzalishaji. Kwa kuongezea zaidi, wakulima wadogo wanahitaji msaada zaidi kuhakikisha kuwa bidhaa wanazozalisha zinakidhi viwango vya ubora vya kimataifa.

Kutatua changamoto hizi, Ubia wa Nyanya umeendelea kufanya kazi kwa karibu na wadau wote wa mradi katika kujenga uwezo wa wakulima wadogo kuzalisha nyanya zinazokidhi kiwango kinachotahitajika. Kampuni za Darsh Industries, Green Valley Agro na wanachama wote katika Ubia huu wanaendelea kutoa msaada wa ziada kwa wakulima wadogo.

Kampuni ya Darsh Industries imetoa kipaumbele kwa wazalishaji wa aina ya nyanya iitwayo 'Tanya' ambayo ina uwezo wa kukaa muda mrefu kabla ya kuharibika, ikimaanisha kuwa inaweza kusafirishwa huku ikbakia katika hali yake bila kuharibika. Hii itasaidia kukabiliana na mapungufu yanayoikabili miundombinu katika eneo la mradi. Ubia unaendelea kushirikana na Serikali na wabia wengine kusaidia ujenzi wa miundombinu katika ukanda. Ubia pia unahakikisha kuwa wakulima wanapata kiasi cha kutosha cha mbegu bora ili waendelee kupanda na kuvuna aina ya nyanya ambayo inatakiwa na msindikaji. Ili kuweza kufikia dhima ya kuwa na mnyororo wa thamani jumuishi na mpana zaidi, ubia unawaomba wanachama muhimu wajitokeze na kushiriki kikamilifu.

## Kwa taarifa zaidi wasiliana nasi kupitia:


SAGCOT Centre Limited

Gholofa ya 5, Jengo la Ikon
Barabara ya Bains, Masaki
S.L.P 80945
Dar es Salaam, Tanzania

**Simu:** +255 22 260 1024
+255 22 260 0146
**Faxi:** +255 22 260 2368

**Barua Pepe:** info@sagcot.co.tz
**Tovuti:** www.sagcot.co.tz


